**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## WIZARA YA KILIMO

# BODI YA KOROSHO TANZANIA

**MWONGOZO WA UHUISHAJI WA KANZIDATA YA WAKULIMA WA ZAO LA KOROSHO NCHINI KWA MWAKA 2024/2025**

**Umeandaliwa na:-**

Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu,
Bodi ya Korosho Tanzania,
S. L. P 533,
**MTWARA.**

***Mwongozo huu umetolewa chini ya Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009 na Kanuni zake za Mwaka 2010***

**Februari, 2025**

## YALIYOMO


YALIYOMO ........................................................ 2

1.0 UTANGULIZI ........................................................ 4

2.0 LENGO LA KUHUISHA KANZIDATA ........................................................ 4

2.1 Lengo Kuu ........................................................ 4

2.2 Malengo Mahsusi ........................................................ 5

3.0 MUDA WA UTEKELEZAJI ........................................................ 5

4.0 TAARIFA ZA MKULIMA ZITAKAZOHUISHWA ........................................................ 5

5.0 MFUMO UTAKAOTUMIKA KUHUISHA TAARIFA ZA WAKULIMA ........................................................ 5

6.0 MADHUMUNI YA MWONGOZO HUU ........................................................ 5

7.0 JINSI UHUISHAJI UTAKAVYOFANYIKA ........................................................ 6

8.0 MBINU ZITAKAZOTUMIKA KUFANIKISHA ZOEZI LA UHUISHAJI ........................................................ 6

9.0 USIMAMIZI NA UFUATILIAJI ........................................................ 7

10.0 NGAZI ZA UTEKELEZAJI NA WAJIBU WA WADAU ........................................................ 7

10.1 Wizara ya Kilimo ........................................................ 7

10.2 Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ........................................................ 7

10.3 Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) ........................................................ 7

10.4 TARI Naliendele ........................................................ 7

10.5 Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) ........................................................ 7

10.6 Sekretarieti ya Mkoa ........................................................ 8

10.7 Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ........................................................ 8

10.8 Vyama Vikuu vya Ushirika ........................................................ 8

10.9 Halmashauri ........................................................ 8

10.10 Maafisa Ugani Kilimo wa BBT Korosho ........................................................ 8

10.11 Maafisa Ugani Kilimo wa Kata na Vijiji ........................................................ 9

10.12 Watendaji wa Kata na Vijiji ........................................................ 9

10.13 Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ........................................................ 9

10.14 Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Mazao (AMCOS) ........................................................ 9

10.15 Wakulima wa Korosho ........................................................ 9

11.0 WAJIBU WA PAMOJA ........................................................ 9

12.0 UFUATILIAJI NA TATHIMINI ........................................................................ 10
13.0 UGHARAMIAJI WA ZOEZI LA KUHUISHA KANZIDATA ..................................... 10
14.0 UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO ................. 10
15.0 HITIMISHO .......................................................................................................... 10

# MWONGOZO WA UHUISHAJI WA KANZIDATA YA WAKULIMA WA ZAO LA KOROSHO NCHINI KWA MWAKA 2024/2025

## 1.0 UTANGULIZI

Serikali imeweka lengo la kuongeza uzalishaji wa korosho ghafi nchini kufikia tani 700,000 msimu wa 2025/2026 na tani 1,000,000 ifikapo mwaka 2029/2030. Sambamba hilo, Serikali inatambua mchango wa takwimu sahihi za idadi ya wakulima na mikorosho, huduma za ugani, na upatikanaji wa pembejeo bora kama nyenzo muhimu katika kufikia malengo ya uzalishaji wa korosho nchini.

Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kwamba kanzidata ya wakulima wa zao la korosho iliyopo inahitaji maboresho ili kuendana na uhalisia. Aidha, mapungufu yaliyopo kwenye kanzidata yalitokana na sababu mbalimbali ikiwemo makarani wasio waadilifu, na udanganyifu wa wakulima wenyewe katika kutoa taarifa za mashamba. Hivyo, maboresho ya kanzidata yatasaidia kupata takwimu sahihi na za uhakika na hatimaye kuisaidia tasnia ya korosho kutekeleza mipango yake ikiwemo uagizaji na usambazaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho kwa wakulima.

Kwa mantiki hiyo, Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali ngazi ya Mikoa na Wilaya, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Kituo cha Naliendele (TARI Naliendele), Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Vyama Vikuu vya Ushirika na Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) imeamua kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho nchini kwa kutumia Mfumo wa Kidijitali uliopo TFRA. Kwa mwaka huu wa 2024/2025 zoezi kuhuisha kanzidata litafanyika katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma (Tunduru), Pwani na Tanga. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo takribani 98% ya wakulima wa korosho nchini wanatoka katika mikoa hiyo. Tofauti na misimu iliyopita katika mwaka huu vijana wa Jenga Kesho Iliyobora ya zao la korosho (BBT Korosho) na Maafisa Ugani Kilimo wa Kata wa Halmashauri ndio watakaohusika moja kwa moja na uhuishaji wa taarifa za wakulima kwenye kanzidata wakishirikiana na maafisa kilimo wa Vyama Vikuu vya Ushirika na viongozi na watendaji wa AMCOS.

## 2.0 LENGO LA KUHUISHA KANZIDATA

### 2.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la uhuishaji wa kanzidata ya wakulima ni kuhakikisha kuwa taarifa za wakulima zinakuwa sahihi, za kisasa na zinaweza kutumika kwa ufanisi katika mipango ya kuendeleza zao la korosho nchini.

### 2.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho nchini ni pamoja na: -

(i) Kuboresha usahihi wa taarifa kwa kuhakikisha taarifa za kila mkulima zinakuwa halisia.
(ii) Kuboresha kanzidata kwa ajili ya kurahisisha uingizaji, uhuishaji (*Update*), uchambuzi na uhifadhi wa taarifa za wakulima wa korosho nchini.
(iii) Kuhakikisha kila mkulima wa zao la korosho anapata namba ya utambulisho atakayoitumia kupata huduma mbalimbali zitolewazo na Serikali ikiwemo pembejeo za ruzuku.
(iv) Kuharakisha upatikanaji wa huduma za kilimo kwa wakulima kwa kuwafikia kwa urahisi.
(v) Kusaidia upangaji wa sera bora za kilimo zinazohusiana na zao la korosho.
(vi) Kuwasajili wakulima wapya wa zao la korosho ambao hawapo kwenye kanzidata ili kuhakikisha kuwa hakuna mkulima anayekosa huduma zinazotolewa na Serikali kwa sababu ya ukosefu wa taarifa zake kwenye kanzidata.
(vii) Kuimarisha uwazi na uwajibikaji kwa kuwa na takwimu sahihi na halisi za wakulima na mahitaji yao.

## 3.0 MUDA WA UTEKELEZAJI

Zoezi la kuhuisha kanzidata kwa mwaka 2024/2025 litatekelezwa kuanzia mwezi Februari hadi Machi, 2025 kwa mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani na kuanzia mwezi Aprili hadi Mei, 2025 kwa Mkoa wa Tanga.

## 4.0 TAARIFA ZA MKULIMA ZITAKAZOHUISHWA

Taarifa za mkulima zitakazohuishwa ni majina matatu ya mkulima, kitambulisho (NIDA/Mpiga Kura) au namba ya mlipa kodi (TIN number) kwa upande wa taasisi, namba ya simu, AMCOS, ukubwa wa shamba, idadi ya mikorosho na umri wake, uzalishaji wa korosho ghafi kwa msimu wa 2024/2025, picha ya mkulima, umiliki wa shamba (La kwake au la kukodi), mahali anapoishi mkulima na mahali lilipo shamba.

## 5.0 MFUMO UTAKAOTUMIKA KUHUISHA TAARIFA ZA WAKULIMA

Zoezi la kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho litafanyika kwa kutumia mfumo wa kidijitali uliopo TFRA. Uhuishaji wa taarifa utafanyika katika ngazi ya kijiji katika Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji ambapo mtaalam anayehusika atawahudumia wakulima mmoja baada ya mwingine.

## 6.0 MADHUMUNI YA MWONGOZO HUU

Madhumuni ya mwongozo huu ni kuweka utaratibu utakaofanikisha zoezi la uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho nchini ikiwa ni pamoja na kuainisha majukumu ya kila mdau katika zoezi zima.

## 7.0 JINSI UHUISHAJI UTAKAVYOFANYIKA

i. Mkulima atatakiwa kwenda katika Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji akiwa na amebeba kitambulisho chake cha uraia (NIDA) au Mpiga kura pamoja na namba yake ya Utambulisho wa Mkulima *(Farmer Identification Number)*;

ii. Mtaalam (BBT Korosho/Afisa Ugani wa Kata/Kijiji) atahuisha taarifa za mkulima kwa kutumia simu janja au kishikwambi kupitia *Application* maalum ijulikanayo *CBT Tool*;

iii. Taarifa za mkulima zitahuishwa kulingana na uhalisia utakaothibitishwa na viongozi wa Serikali ya Kijiji ambacho shamba lipo;

iv. Ujumbe wa neno la siri *(One Time Password – OTP)* utatumwa kwenye simu ya mkulima ili aweze kuthibitisha taarifa zilizohuishwa kwenye kanzidata kuwa ni za kwake na ni sahihi;

v. Endapo taarifa hazipo sahihi afisa ataziboresha kabla ya kutuma katika mfumo na endapo taarifa zipo sahihi zitatumwa katika mfumo na zoezi litakuwa limekamilika kwa mkulima husika; na

vi. Kwa wakulima ambao hawakuwahi kusajiliwa katika mfumo wa usajili wa kidijitali watasajiliwa kama wakulima wapya chini ya uthibitisho wa kimaandishi kutoka kwa mtendaji wa kijiji husika.

## 8.0 MBINU ZITAKAZOTUMIKA KUFANIKISHA ZOEZI LA UHUISHAJI

Ili kufanikisha uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho nchini, utaratibu ufuatao utatumika: -

i. Kufanya vikao vya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wenyeviti wa Halmashauri na Wakurugenzi wa Halmashauri kwa lengo la kujenga uelewa. Aidha, vikao kama hivyo vitafanyika vikihusisha Makatibu Tawala Wasaidizi Uchumi na Uzalishaji, Washauri wa Kilimo Mkoa (RAA), Wakuu wa Idara ya Kilimo wa Halmashauri, Vyama Vikuu vya Ushirika na TARI Naliendele. Pia, vikao kama hivyo vitafanyika katika ngazi ya Kata na Vijiji vikihusisha watendaji wa kata, watendaji wa vijiji na viongozi na watendaji wa AMCOS;

ii. Kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa kidijitali wa usajili wa wakulima kwa maafisa kilimo wa BBT-Korosho, maafisa kilimo wa Kata na Kijiji wa Halmashauri na Vyama Vikuu vya Ushirika;

iii. Kuitisha mikutano ya wakulima wa korosho katika vijiji kwa lengo la kuwajengea uelewa na kuwahamasisha kujitokeza katika zoezi la kuhuisha taarifa zao kuhusu kilimo cha korosho ikiwa ni maandalizi ya usambazaji na ugawaji wa pembejeo za ruzuku msimu wa 2025/2026;

iv. Kupiga mbiu kwa lengo la kuwakumbusha wakulima kuhuisha taarifa zao za kilimo cha korosho kwa wakati kama ratiba itakavyokuwa imetolewa na Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji husika; na

v. Kutumia redio jamii kuelimisha na kuwakumbusha wakulima umuhimu wa kuhuisha taarifa zao kwenye kanzidata ya wakulima wa korosho nchini.

## 9.0 USIMAMIZI NA UFUATILIAJI

Wataalam kutoka Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na wataalam ngazi ya Mkoa na Halmashauri, watasimamia na kufuatilia kwa karibu zoezi la uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho.

## 10.0 NGAZI ZA UTEKELEZAJI NA WAJIBU WA WADAU

### 10.1 Wizara ya Kilimo

i. Kusimamia na kuhakikisha sera zinazohusu usajili wa wakulima nchini zinatekelezwa katika uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho nchini; na
ii. Kutoa maelekezo yenye lengo la kuongeza ufanisi wa zoezi la uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho nchini.

### 10.2 Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)

i Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kutatua changamoto mbalimbali za kimfumo/kiufundi zinazojitokeza katika mfumo wa kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho na kuzitatua kwa haraka**.**

### 10.3 Bodi ya Korosho Tanzania (CBT)

i. Kutoa mafunzo ya uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho kwa maafisa ugani kilimo wa BBT Korosho, maafisa ugani kilimo wa Kata na Vijiji, Maafisa kilimo wa Vyama Vikuu vya Ushirika;
ii. Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa zoezi la uhuishaji wa kanzidata linakuwa na ufanisi;
iii. Kusitisha usajili wa wakulima watakaobainika kugushi taarifa ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua kwa maafisa waliohusika na uhuishaji/usajili husika;

### 10.4 TARI Naliendele

Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kutoa mafunzo ya uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho kwa maafisa watakaohusika na zoezi hilo katika Halmashauri husika.

### 10.5 Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)

Kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinavyohusika na zao la korosho vinatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa Mwongozo huu.

### 10.6 Sekretarieti ya Mkoa

i. Kuzielekeza Halmashauri kushiriki kikamilifu katika kufanikisha zoezi la uhuishaji wa kanzidata ya wakilima wa korosho;
ii. Kufanya ufuatiliaji kwa Halmashauri juu ya ushiriki wao katika zoezi hili;
iii. Kuhamasisha wakulima wa korosho kujitokeza kuhuisha taarifa zao za kilimo cha korosho; na
iv. Kuchukua hatua za haraka kwa Halmashauri zitakazoonesha uzembe au ushiriki hafifu katika kufanikisha zoezi la uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho.

### 10.7 Ofisi ya Mkuu wa Wilaya

Kuhamasisha wakulima wa korosho kujitokeza kuhuisha taarifa zao za kilimo cha korosho.

### 10.8 Vyama Vikuu vya Ushirika

i. Kuhamasisha wakulima wa korosho kujitokeza kuhuisha taarifa zao za kilimo cha korosho; na
ii. Kusimamia AMCOS kuhakikisha kuwa zinatoa ushirikiano katika zoezi la kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho katika maeneo yao.
iii. Maafisa kilimo wake kushirikiana na maafisa kilimo wa BBT Korosho kuhuisha taarifa za wakulima kwenye kanzidata.

### 10.9 Halmashauri

i. Kufanya uhamasishaji kwa wakulima juu ya umuhimu wa kujitokeza katika zoezi la kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho;
ii. Kusambaza mwongozo huu kwa Watendaji wa Kata na Vijiji ili waweze kuwajibika ipasavyo;
iii. Kufanya ufuatiliaji wa maendeleo ya zoezi la uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho; na
iv. Kutoa taarifa za mwenendo wa usajili kwa Sekretariati za Mikoa na Ofisi za Wakuu wa Wilaya.

### 10.10 Maafisa Ugani Kilimo wa BBT Korosho

i Kuhuisha taarifa za wakulima wa korosho kwenye kanzidata kwa kutumia mfumo wa kidijitali uliopo TFRA;
ii Kupokea na kuzingatia mafunzo yatakayotolewa juu ya zoezi la kuhuisha taarifa za wakulima wa korosho kwenye kanzidata;
iii Kushirikiana na viongozi wa Kata na Vijiji katika kuhamasisha wakulima kujitokeza kuhuisha taarifa zao za kilimo cha korosho; na
iv Kuhakikisha wakulima waliopo kijijini wanapata taarifa juu ya zoezi la kuhuisha kanzidata ya wakulima.

### 10.11 Maafisa Ugani Kilimo wa Kata na Vijiji

i. Kushirikiana na maafisa ugani kilimo wa BBT Korosho kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho;
ii. Kusimamia na kuhakikisha kuwa mwongozo huu unaeleweka vema kwa wakulima;
iii. Kushirikiana na viongozi wa Kata na Vijiji katika kuhamasisha wakulima kujitokeza kuhuisha taarifa zao za kilimo cha korosho; na
iv. Kuhakikisha wakulima waliopo kijijini wanapata taarifa juu ya zoezi la kuhuisha kanzidata ya wakulima.

### 10.12 Watendaji wa Kata na Vijiji

i. Kuhamasisha wakulima kuhuisha taarifa zao za kilimo cha korosho;
ii. Kufanya ufuatiliaji wa zoezi la kuhuisha kanzidata ya wakulima katika Kata/Kijiji husika;
iii. Kuwasilisha changamoto zilizoshindwa kupatiwa ufumbuzi ngazi ya Kijiji/Kata kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika; na
iv. Kushirikiana na maafisa kilimo wa Bodi ya Korosho, wa Halmashauri na wa Vyama Vikuu vya Ushirika wakati wote wa zoezi la kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho.

### 10.13 Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji

Kushiriki kikamilifu katika zoezi la kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho kwa kutekeleza mambo yafuatayo: -

i. Kuhamasisha wakulima katika maeneo yao kujitokeza kuhuisha taarifa za mashamba kwenye kanzidata ya wakulima wa korosho; na
ii. Kutoa ushirikiano kwa maafisa kilimo katika zoezi la kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korisho katika maeneo yao.

### 10.14 Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Mazao (AMCOS)

i Kuhamasisha wakulima katika maeneo yao kujitokeza kuhuisha taarifa za mashamba kwenye kanzidata ya wakulima wa korosho; na
ii Kutoa ushirikiano kwa maafisa kilimo katika zoezi la kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korisho katika maeneo yao.

### 10.15 Wakulima wa Korosho

i. Kujitokeza kwa ajili ya kuhuisha taarifa za kilimo cha korosho; na
ii. Kutoa taarifa sahihi zitakazohitajika kwenye kanzidata ya wakulima wa korosho.

## 11.0 WAJIBU WA PAMOJA

i. Kuhakikisha majukumu haya yanatekelezwa kwa kuzingatia sera na sheria za nchi;

ii. Kutoa taarifa mapema kuhusu suala lolote ambalo litakwamisha utekelezaji wa Mwongozo huu; na
iii. Kuhakikisha kila mdau husika anatimiza wajibu wake.

## 12.0 UFUATILIAJI NA TATHIMINI

Ufuatiliaji na tathmini ya zoezi zima la kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho utafanywa na wataalamu kuanzia mwanzo hadi mwisho wa zoezi la kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho nchini.

## 13.0 UGHARAMIAJI WA ZOEZI LA KUHUISHA KANZIDATA

Kwa kuwa wahusika katika zoezi hili la uhuishaji wa kanzidata ya wakulima kwa namna moja ama nyingine ni wanufaika *(Beneficiaries)* wa zao la korosho hapa nchini; kila mmoja atatakiwa kujigharamia kupitia Ofisi yake ili kuweza kufikia malengo ya uzalishaji wa korosho ghafi tani 700,000 msimu wa mwaka 2025/2026.

## 14.0 UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO

Endapo kutatokea changamoto yoyote juu ya uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho iwasilishwe na kushughulikiwa kulingana na ngazi ya utekelezaji kuanzia Kijiji, Kata, Halmashauri, Mkoa na Bodi ya Korosho Tanzania. Aidha, Bodi ya Korosho Tanzania imeandaa namba ya simu ya bure ambayo ni ***0 8 0 0 1 1 2 1 5*** **9** kwa ajili ya kupokea maoni, ushauri, changamoto na kushughulikia kulingana na ngazi husika

## 15.0 HITIMISHO

Kutokana na ukweli kwamba, kanzidata iliyopo ina taarifa nyingi za wakulima ambazo zinahitaji kuhuishwa ili kuendana na uhalisi kwa mwaka huu wa 2024/2025; zoezi hili lichukuliwe kwa umuhimu mkubwa na lifanyike kwa wakati ili usambazaji wa pembejeo na maamuzi mengine katika uzalishaji wa korosho yafanyike kwa wakati kwa maslahi mapana ya maendeleo ya Tasnia ya Korosho nchini.

Mwongozo huu umetolewa na kusainiwa leo tarehe **12 Februari, 2025.**

Francis Alfred
**Mkurugenzi Mkuu**
Bodi ya Korosho
Tanzania